# Tanzania PANORAMA

UNAPOHITAJI UKWELI ILI UWE HURU

# WASIFU WA KAMPUNI



## Dira Yetu

Kuwa chombo cha habari cha mtandaoni kinachoongoza Tanzania kwa kutoa taarifa sahihi, za kuaminika na zenye utafiti wa kina, na kuwa kiungo imara cha mawasiliano kati ya Serikali, taasisi mbalimbali na wananchi.

## Dhamira Yetu

Kutoa habari sahihi na zilizothibitishwa kwa wakati, kwa kuzingatia weledi na uhuru wa uandishi wa habari, ili kulinda maslahi ya umma, kukuza uwajibikaji na kuiwezesha jamii kupata taarifa zinazowawezesha kufanya maamuzi sahihi kwa mustakabali bora wa nchi

## Maadili ya Msingi

Tunaongozwa na maadili ya msingi yanayojumuisha uhuru wa habari, usahihi na uhakiki wa taarifa, uadilifu na uwajibikaji, ubunifu unaoendana na matumizi ya teknolojia ya kidijitali, pamoja na wajibu kwa jamii. Aidha, tunazingatia uwazi na usawa katika uandishi wa habari ili kuhakikisha tunatoa taarifa zenye kuaminika, zenye mizani na zinazolenga maslahi ya umma.

Baadhi ya Washirika Wetu

NHC · TPA · Hifadhi za Taifa Tanzania National Parks



## Kutoka kwa Mkurugenzi Mtendaji

Katika ulimwengu wa habari unaobadilika kwa kasi, Tanzania Panorama Blog, tunadhamiria kuwa vinara katika uandishi wa habari unaozingatia uhuru, usahihi, uwajibikaji, maslahi ya umma na usalama wa taifa letu lenye historia ya kipekee, utamaduni tajiri, rasilimali nyingi na fursa kubwa za maendeleo.

Tanzania PANORAMA Blog tunabeba jukumu la kuhabarisha umma kuhusu masuala muhimu yanayogusa maisha ya wananchi na nchi yakiwemo ya maendeleo ya kiuchumi, kijamii, uongozi, utawala bora, pamoja na fursa mbalimbali za kitaifa na kimataifa.

Tunaamini kuwa uandishi wa habari ni huduma kwa umma, hivyo tumejitoa kutumikia jamii ya Watanzania kwa uadilifu, uwazi, na weledi wa hali ya juu.

Timu yetu ya wanahabari na wahariri wenye uzoefu ina dhamira ya kuwa kiunganishi kati ya Serikali, taasisi, na wananchi kwa kuripoti habari kwa usawa na kwa misingi ya taaluma. Aidha, tumedhamiria pia kuhimiza utamaduni wa kufikiri kwa kina, kutoa nafasi ya mawazo tofauti yenye heshima, na kusimamia ukweli kupitia uchunguzi na uthibitishaji wa taarifa.

Tunawashukuru Watanzania, wadau na washirika wetu kwa ujumla kwa kutuamini na kutuchagua kama chanzo chao cha kuaminika cha kuhabarika.

Tutaendelea kushirikiana nanyi katika kujenga taifa lenye taarifa sahihi na lenye maamuzi bora kwa maendeleo ya jamii.

**Charles Mullinda**
**Mkurugenzi Mtendaji**

## KWA UFUPI KUHUSU TANZANIA PANORAMA

Tanzania PANORAMA Blog ni jukwaa la habari mtandaoni linalojikita katika kuripoti taarifa sahihi, za kuaminika na zenye kufanyiwa utafiti wa kina kuhusiana na Tanzania na ulimwengu kwa ujumla.

Kupitia uandishi wetu wa habari wa kiweledi, kitaalamu, uchambuzi wa kina, na matumizi ya teknolojia ya kidijitali, Tanzania PANORAMA Blog imejiimarisha kama chombo huru cha habari kinacholenga kutoa taarifa kwa wakati na kwa uadilifu.

Tunatambua kuwa taifa lenye wananchi wenye uelewa wa taarifa sahihi huwa na msingi ulio imara wa demokrasia, maendeleo ya kiuchumi, na ustawi wa kijamii na Tanzania PANORAMA Blog ipo kwa ajili ya kuhabarisha, kuelimisha na kuchochea mijadala yenye tija kwa maendeleo ya Taifa.

Kwa kuzingatia maadili na weledi wa uandishi wa habari, tunahakikisha taarifa zetu zinapitia mchakato wa uhakiki na uhariri kwa lengo la kuimarisha ukweli, uwazi na uwajibikaji.

Sambamba na hilo, tunawekeza katika ubunifu wa maudhui ya kidijitali kupitia maandishi, picha, video na utiririshaji wa moja kwa moja (live streaming) ili kufikisha habari kwa haraka, kwa urahisi na kwa namna inayoendana na mahitaji ya hadhira ya kisasa.

## HUDUMA ZITOLEWAZO NA TANZANIA PANORAMA BLOG

**01** **Uandishi na Uchambuzi wa Habari Mtandaoni**
Utoaji wa habari, makala maalum, na uchambuzi wa kitaalamu kwa maandishi.

**02** **Utayarishaji wa Video, Makala Na Vipindi Mbalimbali**
Ripoti katika mtindo wa picha mjongeo, mahojiano, makala na taarifa za matukio mbalimbali.

**03** **Utiririshaji wa Moja kwa Moja (Live Streaming)**
Matangazo ya moja kwa moja ya matukio ya kitaifa, mikutano, na shughuli maalum.

**04** **Utoaji wa Habari kupitia Mitandao ya Kijamii**
Kusambaza habari kwa haraka kupitia majukwaa ya kijamii ili kuongeza ufikiaji wa wateja wetu

**05** **Matangazo na Uhamasishaji (Advertising & Promotions)**
Kutoa nafasi ya matangazo ya biashara, taasisi na kampeni za kijamii kwa kufuata maadili

## Maeneo ya Maudhui (Content Coverage)

Tanzania PANORAMA Blog huzalisha na kusambaza maudhui katika maeneo yafuatayo:

**i. Breaking News**
Habari za papo kwa papo kuhusu matukio makubwa ya kitaifa na kimataifa.

**ii. Siasa na Utawala Bora**
Taarifa na uchambuzi wa masuala ya kisiasa, uchaguzi, sera na uongozi.

**iii. Uchumi na Biashara**
Habari za uchumi, biashara, uwekezaji, masoko, fedha, utalii na fursa za maendeleo.

**iv. Jamii na Maendeleo**
Habari za afya, elimu, mazingira, haki za binadamu, na ustawi wa jamii.

**v. Michezo na Burudani**
Taarifa kuhusu michezo ya ndani na kimataifa pamoja na burudani na sanaa.

**vi. Maoni na Uchambuzi**
Makala za uchambuzi na mitazamo tofauti kuhusu masuala ya sasa kwa kuzingatia heshima na ukweli.

**vii. Vipengele Maalum na Uchunguzi (Investigative Journalism), ripoti za kina kuhusu masuala nyeti yanayogusa maslahi ya umma, kwa ushahidi na utafiti wa kitaalamu.**

## Malengo ya Kimkakati (Strategic Objectives)

**Kuimarisha kiwango cha ubora wa uandishi wa habari kwa kuzingatia viwango vya kitaalamu.**

**Kuongeza ufikiaji wa habari kupitia majukwaa ya kidijitali na mitandao ya kijamii.**

**Kukuza maudhui ya uchunguzi, mahojiano, na taarifa za kina zenye ushahidi.**

**Kuwa daraja la mawasiliano kati ya wananchi na mamlaka husika.**

**Kutoa taarifa zinazosaidia wawekezaji, wafanyabiashara na wadau wa maendeleo kufanya maamuzi sahihi.**

**Kujenga mfumo imara wa maudhui unaozingatia maadili, sheria za habari, na ulinzi wa taarifa.**

## Walengwa (Target Audience)

**Tanzania PANORAMA Blog inawahudumia wasomaji na watazamaji mbalimbali wakiwemo:**

**Wananchi wa Tanzania wanaotafuta habari za ndani na kitaifa**

**Jumuiya ya kimataifa inayohitaji taarifa kuhusu Tanzania**

**Wafanyabiashara, wawekezaji na taasisi za fedha**

**Watunga sera, wanazuoni, watafiti na wanafunzi**

**Wanasiasa, wanadiplomasia na viongozi wa umma**

**Mashirika ya kiraia, taasisi za dini, na jamii kwa ujumla**

## Sera ya Uhariri na Uhakiki wa Taarifa (Editorial & Fact-Checking Policy)

Ili kulinda uaminifu wa chombo chetu, Tanzania PANORAMA Blog inazingatia misingi ifuatayo:

i. Kuhakikisha taarifa zinathibitishwa kabla ya kuchapishwa (fact-checking).

ii. Kutenganisha habari, maoni, na matangazo ili kuepuka upotoshaji.

iii. Kutoa haki ya kusikilizwa kwa pande zote (balanced reporting).

iv. Kuheshimu sheria za habari, faragha, na maadili ya taaluma.

v. Kufanya marekebisho (corrections) wazi pale taarifa inapobainika kuwa na makosa.

vi. Kuzuia lugha ya chuki, uchochezi, au maudhui yanayokiuka misingi ya amani na umoja wa kitaifa.

## Teknolojia na Ubunifu (Innovation & Digital Strategy)

Tanzania PANORAMA Blog inawekeza katika teknolojia ili kuongeza ubora wa huduma kwa hadhira, ikiwemo:

Matumizi ya mifumo ya kisasa ya kuchapisha habari (CMS)

Ulinzi wa taarifa na usalama kidijitali (cyber security)

Uboreshaji wa SEO na digital analytics kufahamu mahitaji ya wasomaji

Kuimarisha maudhui ya picha mjongeo (videos), podcasts na infographics

Kuongeza matumizi ya mobile content na short-form content kwa mitandao ya kijamii

## Ushirikiano na Wadau (Partnerships)

Tanzania PANORAMA Blog tunashirikiana na taasisi, mashirika na vyombo mbalimbali vya habari ili kuongeza ubora wa taarifa na kufikia hadhira pana zaidi.

Chombo hiki kimejenga ushirikiano na taasisi mbalimbali za umma na binafsi kwa madhumuni ya:

- kutoa taarifa sahihi na kwa wakati
- kuhamasisha maendeleo ya jamii
- kuboresha upatikanaji wa maudhui

Tunawashukuru wadau wetu wote ambao wametuamini kama chanzo chao kikuu cha kupata habari na wale ambao wametuamini na kukubali kufanya kazi nasi.

## MAJUKWAA YA KIDIJITALI (DIGITAL PRESENCE)

**Tanzania PANORAMA Blog**
ina uwepo mkubwa mtandaoni kupitia:

**Tovuti rasmi (Website)**
yenye muonekano rafiki kwa mtumiaji (mobile friendly)

**Mitandao ya kijamii**
Facebook, Instagram, X/Twitter, YouTube, TikTok n.k.

**Maudhui ya video na vipindi**
kupitia Tanzania Panorama Online TV

**Live streaming kwa matukio,**
mikutano ya waandishi wa habari na shughuli za kijamii

**Vipengele wasilianifu**
kama maoni ya wasomaji, poll, na ushiriki wa jamii

### Washirika Wetu

**Tanzania Panorama Blog | Ofisi ya Makao Makuu**
**Mtaa wa Samora, Jengo la Kitegauchumi, Ghorofa ya 11**
**S. L. P. 1000026 Dar es Salaam | Simu: +255 711 464 984 | Baruapepe: info@tanzaniapanorama.com**